


# Kenya: Mustakabali wa Usaidizi wa Kijamii ni upi chini ya Utawala wa Ruto?

Rachel Strohm

Makala ya Sera Namba 1
13 Septemba 2022

Social Policy Insights

## Ufupisho

Je, Rais mpya wa Kenya William Ruto yuko tayari kuimarisha mipango ya kutoa usaidizi wa kijamii kwa maskini hasa wakati huu ambao Wakenya wanaendelea kukabiliwa na gharama za maisha kupanda?

Ilani ya rais mpya inaonyesha ufahamu wa mahitaji ya usaidizi zaidi wa kijamii, lakini ina upungufu wa ahadi maalum.

*Zingatia: Makala haya yalichapishwa kwa mara ya kwanza kwa Kiingereza na African Arguments.*[1] *Tunawashukuru Global Voices Translation Services (https://globalvoices.org) na Kanyi Wyban kwa tafsiri.*

## Kuhusu Mwandishi

Rachel Strohm ni mkurugenzi wa Social Policy Insights. Awali, alikuwa mkurugenzi mshirikishi wa ulinzi wa jamii katika Innovations for Poverty Action, na mwasisi mwenza wa Mawazo Institute. rachel@socialpolicyinsights.org

## Kuhusu Mchapishaji

Social Policy Insights ni shirika la utafiti lililopo Nairobi, Kenya. Tunasaidia watekelezaji wa sera za kijamii na wafadhili kuelewa kuhusu kinachofaa kuimarisha mipango yao, na kutoa njiasahihi na jumuishi ya ulinzi wa kijamii kwa wanaolengwa kunufaika kote Afrika Mashariki. https://socialpolicyinsights.org

*Picha ya Jalada: Bango la kampeni la Kenya Kwanza, 2022 (Simon Maina, AFP/Getty Images)*

[1] "Kenya: What Future for Social Assistance Under Ruto?" 13 September 2022. *African Arguments*. https://africanarguments.org/2022/09/kenya-what-future-for-social-assistance-under-ruto/

## Utangulizi

Kupanda kwa gharamaza maisha kumesababisha raia wa kawaida kuandamana barabarani mwaka huu. Mara nyingine, maandamano haya huwa na sababu maalumukama yale ya Julai ambayo yalitaka mageuzi kuhusiana na masuala ya njaa ili kupunguza bei za vyakula (Mathare Social Justice Centre 2022). Wakati mwingine, watu wamejeruhiwa barabarani bila kukusudiwa, wakiwa wanasubiri ndani ya magari yao kwa muda mrefu kutokana na upungufu wa mafuta (Mjahid 2021).

Ingawa ukuaji wa uchumi umeanza kuinuka tena baada ya janga la Covid-19 nchi bado imelazimika kuvumilia miaka mingi ya kiangazi kikali, usimamizi mbovu wa uchumi na kuongezeka kwa bei za bidhaa kutokana na vita vya nchini Ukraine (BBC 2022A, Guguyu 2022, Kamau 2022, Ngugi 2021).

Katika uchunguzi wa hivi karibuni wa Afrobarometer (2022), zaidi ya asilimia 80 ya Wakenya waliohojiwa walisema hali ya uchumi wa kitaifa “ni mbaya kiasi” au “mbaya sana”. Wengi walisema kuwa mara nyingi hukosa bidhaa za msingi na huduma, kama chakula cha kutosha (18%), maji safi (22%) matibabu (26%), au mapato ya kifedha (47%).

Mipango ya kutoa usaidizi kwa jamii inaweza kuwasaidia raia waliopo hatarini zaidi wakati wa mizozo (Carter et al. 2019). Mpango huu husaidia kiuchumi, kama kusambaza fedha, kwa wanaonufaika na mpango, bila kuwahitaji wao kuchangia chochote. Ni mipango ambayo haihusishi watu kupata pesa kulingana na michango yao.

Ni tofauti na mipango ya kijamii ya bima, ambayo inajumuisha bima ya kutokuwa na ajira au afya, na inahitaji wahusika kulipa kwanza na kupata manufaa yake baadaye- kwa lugha nyingine ni kuwa ni “mpango wa kuchangia fedha”.

Kwa sababu mipango ya kusaidia jamii haihitaji wanaonufaika kulipa chochote, huwa ni chaguo bora la kutoa usaidizi wa kiuchumi kwa familia ambazo ni maskini sana.

Wakati huu ambao William Ruto ameapishwa kuchukua madaraka baada ya Mahakama ya juu kudumisha ushindi wake wa uchaguzi wa Agosti 9 (BBC 2022B), ni usaidizi gani wa kijamii ambao Wakenya wa kawaida huenda wakatarajia kutoka kwa utawala wa Kenya Kwanza?

## Mipango ya usaidizi wa kijamii nchini Kenya

Ruto alianzakuwa mtumishi wa umma kwanza kama mbunge kutoka 1998-2013, na kisha naibu wa rais chini ya Rais Uhuru Kenyatta kuanzia 2013-2022, ni kipindi ambacho kimeshuhudia ongezeko la mipango ya kutoa usaidizi kwa jamii (BBC 2021).

Tangu 2003, Kenya imekuwa ikitoa msaada wa kifedha kwa nyumba maskini zaidi kupitia mpango wa Kitaifa wa National Safety Net Programme (NSNP),[2] ambao pia unafahamika kama Inua Jamii (Luchi 2022). Mipango iliyopo sasa inajumuisha mayatima na watoto wanaoishi mazingira hatarishi, watu wenye ulemavu, watu walioathiriwa na kiangazi katika maeneo yenye ukame, na raia wote wenye umri wa zaidi ya miaka 70.

Katika shughuli zake za takribani miongo miwili, NSNP imeshuhudia ufanisi. Kufikia mwaka 2019, nyumba zaidi ya 1.3 milioni zilikuwa zimesajiliwa kwenye mpango huo wa kuzijali, ambapo takriban watu 5 milioni au 10% ya idadi ya watu (ILO 20223, Ministry of Labour and Social Protection [MLSP] 2017). Zaidi ya hayo, mpango huo husambaza pesa hizo kidijitali hatua inayopunguza ulaghai, na kufadhiliwa kikamilifu na mapato yake ya ushuru wa ndani badala ya pesa za wafadhili (Baswony et al. 2022, MLSP 2017).

Hata hivyo, kuna nafasi kwa NSNP kuimarisha shughuli zake. Muhimu zaidi, idadi ya wanaosajiliwa kwa mpango huo ni chini ya iliyokadiriwa ya 33.4% ya idadi ya jumla ya watu (ambayo ni takriban watu milioni 17) ambao bado wanaishi katika hali maskini kwa chini ya dola moja na senti 90 kufikia 2022 (World Bank 2022).

## Ilani ya Kenya Kwanza: Maelezo mbalimbali kuhusu usaidizi wa kijamii

Utawala wa Ruto unapanga kuimarisha vipi uwezo wa NSNP na kushughulikia mapungufu yake?

Tathmini ya ilani ya muungano wa kisiasa wa Kenya Kwanza inaonyesha kuwa Ruto anafahamu haja ya kuongeza misaada ya kijamii, lakini hajatoa hakikisho maalum la kuimarisha mipango ya kusambaza fedha (Kenya Kwanza 2022).

Ilani hiyo inaeleza kuwa Wakenya wanakabiliwa na athari nyingi za maisha, ambazo ni pamoja na umaskini miongoni mwa watoto, wazee na watu wenye ulemavu. Mipango iliyopo sasa ya misaada ya kijamii inafikia 7.5% tu kwa watoto wanaoishi katika umaskini, kulingana na takwimu zao.

Zaidi ya hayo, ilani hiyo inaeleza kuwa karibu 85% ya wafanyakazi ambao ni watu wazima wako katika sekta isiyo rasmi ya ajira (jua kali) (Federation of Kenya Employers 2021). Hii inamaanisha kuwa wanakosa kunufaika na bima za kijamii ambazo zipo katika ajira rasmi, kwa sababu waajiri wanahitajika kuchangia 50% ya malipo ya Bima ya Matibabu (National Hospital Insurance Fund / NHIF) kwa waajiri wao (Sundays 2022).

[2] "National Safety Net Programme." National Social Protection Secretariat. https://www.socialprotection.or.ke/social-protection-components/social-assistance/national-safety-net-program

Hii inaonyesha wazi changamoto ya umaskini nchini Kenya. Hata hivyo, haiendani na pendekezo la wazi la sera ya kutumia usaidizi wa kijamii kupunguza umaskini.

Ilani (manifesto) hiyo inaitaka serikali kuanzisha "mfumo wa usalama wa kijamii kwa wote, ambao unajumuisha pensheni, bima ya hali ya hatari kazini na kukosa ajira." Lakini haielezi ikiwa hii itaongeza au kuchukua nafasi ya pensheni ya kijamii kwa wote – kwa watu wenye umri wa zaidi ya miaka 70, ambayo tayari inatolewa kupitia NSNP (Chirchir & Tran 2019).

Kuongeza wingi wa upatikanaji wa bima ya hali ya hatari kazini na ukosefu wa ajira ni wazo zuri, lakini pia haiko wazi jinsi pendekezo hili litatatua shida za kimsingi kwa wafanyakazi wa juakali: watamudu vipi gharama za ada za bima.

Ilani hiyo pia haisemi mengi kuhusu mpango wa sasa wa kusambaza fedha, mbali na ahadi ya "kuimarisha uendeshaji wa shughuli zake, uwajibikiaji malipo upesi na maeneo yanayohusika."

Mpinzani wake Ruto katika uchaguzi uliofanyika Agosti 9 – Raila Odinga wa Muungano wa Azimio la Umoja – alifanya kampeni ya kuimarisha wanaosajiliwa kwa msaada wa kijamii kwa 50% na kuongezeka mara tatu ya kiasi cha fedha kinachotolewa kwa mwezi (Azimio la Umoja 2022). Ruto aliepuka kuelezea kwa kikamilifu ahadi ya aina hii ya kuongeza msaada wa kijamii.

Hata hivyo, Kenya Kwanza inaleta wazo moja la kipekee mezani: kuanzisha mfumo wa maslahi ya kijamii kwa Wakenya wanaoishi nje, kwa kuangalia na kutekeleza uwezekano waulinzi wa kijamii. Wakenya wengi ughaibuni wanakabiliwa na mazingira mabovu ya kikazi na wanakosa kufikia mifumo ya kitaifa ya ulinzi wa kijamii katika nchi wanazoishi, na wazo hili ni zuri la kufuatilia (Malit & Al Youha 2016).

Hatimaye, utawala wa Ruto unaonekana kulenga kuongeza bima ya kijamii badala ya msaada wa kijamii. Hii ina hatari ya kupunguza hatua zilizopigwa na NSNP katika miongo miwili iliyopita, na huenda ikasababisha nyumba zaidi zilizopo kwenye hatari kukosa msaada.

## Kazi Zilizotajwa


Afrobarometer. 2022. "News Release: Kenyans See Worsening Economic Conditions, Cite Poor Government Performance, Afrobarometer Survey Shows." https://www.afrobarometer.org/wp-content/uploads/2022/04/news_release-kenyans_see_worsening_economic_conditions_cite_poor_government_performance-1march22.pdf.

Azimio la Umoja. 2022. "Azimio La Umoja One Kenya Coalition Inewezekana Agenda 2022-2017." https://www.socialpolicyinsights.org/s/AZIMIO-MANIFESTO-compressed.pdf.

Baswony, Collins et al. 2022. "Drought, Digital Innovation, and Money: How the Hunger Safety Net Cash Transfer Programme Has Transformed Access to Financial Services in the Arid Lands of Kenya." Financial Sector Deepening Kenya. https://www.fsdkenya.org/blogs-publications/blog/drought-digital-innovation-and-money-how-the-hunger-safety-net-cash-transfer-programme-has-transformed-access-to-financial-services-in-the-arid-lands-of-kenya/.

BBC. 2021. "William Ruto: Muuza kuku aliyepanda ngazi hadi kuwa rais wa Kenya." *BBC News Swahili*. https://www.bbc.com/swahili/habari-58174625.

———. 2022a. "Kupanda kwa bei ya vyakula kumezua ghadhabu nchini Kenya." *BBC News Swahili*. https://www.bbc.com/swahili/habari-60489007.

———. 2022b. "Matokeo ya Uchaguzi Kenya 2022: M ahakama ya juu yamuidhinisha rais mteule William Ruto kuwa mshindi wa uchaguzi mkuu." *BBC News Swahili*. https://www.bbc.com/swahili/articles/c72wwrww4vvo.

Carter, Becky, Keetie Roelen, Sue Enfield, and William Avis. 2019. "Social Protection Topic Guide." Institute for Development Studies, University of Sussex. https://opendocs.ids.ac.uk/opendocs/bitstream/handle/20.500.12413/14885/Social_Protection_Topic_Guide_online.pdf?sequence=1&isAllowed=y.

Chirchir, Richard, and Tran Anh. 2019. "Kenya - Inua Jamii Senior Citizens' Scheme." ILO Social Protection Platform. https://www.social-protection.org/gimi/RessourcePDF.action?id=55525.

Federation of Kenya Employers. 2021. "The Informal Economy in Kenya." https://www.ilo.org/wcmsp5/groups/public/---ed_emp/---emp_ent/documents/publication/wcms_820312.pdf.

Guguyu, Otiato. 2022. "Half a Million Kenyans out of Extreme Poverty." *Business Daily*. https://www.businessdailyafrica.com/bd/economy/half-a-million-kenyans-out-of-extreme-poverty-3812372.

International Labour Organization. 2023. "Kenya County Profile." ILO Social Protection Platform. https://www.social-protection.org/gimi/ShowCountryProfile.action?iso=KE.

Kamau, Wanderi. 2022. "NJENJE: Kiangazi Kinachoendelea Chanyima Kenya Nafasi Ya Kuuza Maziwa Yake Oman." *Nation*. https://taifaleo.nation.co.ke/njenje-kiangazi-kinachoendelea-chanyima-kenya-nafasi-ya-kuuza-maziwa-yake-oman/.

Kenya Kwanza. 2022. "The Kenya Plan: The Bottom-Up Economic Transformation Agenda 2022-2027." https://www.socialpolicyinsights.org/s/Kenya-Kwanza-manifesto-2022-compressed-1.pdf.

Luchi, Athman. 2022. "Serikali Yatoa Pesa Za Wazee Chini Ya Mpango Wa Inua Jamii Cash Transfer." *Radio Rahma*.

https://radiorahma.co.ke/news/index.php/angazo/614-serikali-yatoa-pesa-za-wazee-chini-ya-mpango-wa-inua-jamii-cash-transfer.

Mahit Jr, Froilan, and Ali Al Youha. 2016. "Kenyan Migration to the Gulf Countries: Balancing Economic Interests and Worker Protection." *Migration Policy Institute*. https://www.migrationpolicy.org/article/kenyan-migration-gulf-countries-balancing-economic-interests-and-worker-protection.

Mathare Social Justice Centre. 2022. "Saba Saba 2022 Edition." https://www.matharesocialjustice.org/elections/saba-saba-2022-edition/.

Ministry of Labour and Social Protection. 2017. "Kenya Social Protection Sector Review." https://www.socialprotection.or.ke/information-center/news-and-events/205-kenya-social-protection-sector-review.

Mjahid, Amina. 2021. "Bei ya mafuta yapanda maradufu nchini Kenya." *DW*. https://www.dw.com/sw/bei-ya-mafuta-yapanda-maradufu-nchini-kenya/a-59192626.

Ngugi, Tee. 2021. "The Real Debt Burden in Kenya Is Corruption." *The East African*. https://www.theeastafrican.co.ke/tea/oped/comment/real-debt-burden-in-kenya-is-corruption-3364482.

Sundays, Purity Ngigi. 2022. "Employers Required to Match Employees NHIF Contributions." Matthew and Partners Advocates LLP. https://matthewandpartnersllp.com/employers-required-to-match-employees-nhif-contributions/.

World Bank. 2022. "Kenya Macro Poverty Outlook." https://documents1.worldbank.org/curated/en/099326404262224251/pdf/IDU0dc51bdb4027df045a40aa24016b4db3ba3e5.pdf.